Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 26.05.2020; Accepted 28.05.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

# Uchanganuzi wa Maudhui na Wahusika Kibibliotherapia katika Hadithi Fupi Teule za Kiswahili

**Rose Mavisi[1]; Dr. Gwachi Mayaka[2]; Prof. Wendo Nabea[3]**
**[1,2,3] Laikipia University, Kenya**
**Main Author Email: rosemasai@gmail.com**

## IKISIRI

Bibliotherapia ni mbinu muhimu inayoweza kutumiwa kama kipumuo kwa vijana kwa baadhi ya matatizo yanayowakumba katika kipindi fulani cha maisha yao. Bibliotherapia humsaidia msomaji kupitia mtagusano wake na maudhui na wahusika ambao wamepitia hali kama ya yule msomaji. Makala haya yalilenga kuchanganua maudhui na uhusika ili kubaini sifa za kibibliotherapia katika diwani hizi za hadithi fupi; *Mayai Waziri wa Maradhi na hadithi nyingine* (2004), *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2007), *Kiti cha Moyoni na hadithi nyingine* (2007) na *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* (2016). Mbinu iliyotumiwa kukusanya data hii ni majadiliano katika makundi au kundi lengani. Utafiti huu ulipata matini yake kutoka kwa hadithi fupi teule zinazotumiwa au zinazoweza kutumiwa kama matini ya fasihi ya Kiswahili katika shule za upili. Utafiti huu ulichukua sampuli kutoka kwa shule 7 za Serikali katika eneo la utafiti. Eneo la utafiti ni kaunti ya Nairobi. Sampuli iliteuliwa kwa kutumia mbinu zifuatazo; kimakusudi, kinasibu na utabakishaji. Watafitiwa walikuwa walimu 28 pamoja na wanafunzi 112 wa Kidato cha Tatu wa fasihi ya Kiswahili ambao walizisoma hadithi fupi teule na kutathmini sifa za kibibliotherapia.Kazi hii iliongozwa na mihimili ya nadharia ya Mapatano ya Mwitikio wa Msomaji yake Rosenblatt (1995). Mijadala ya kundi lengani ilionyesha kwamba hadithi fupi zinazosomwa darasani ni za kuaminika na maudhui yanaeleweka vizuri .Ufaafu wa maudhui na wahusika kwa mahitaji ya wanafunzi ni muhimu ili faida za kibibliotherapia zipatikane.

**Maneno muhimu**: *bibliotherapia, maudhui, wahusika na uhusika.*

**How to cite this article in APA (6th Edition)**

Mavisi, R., Mayaka, G., & Nabea, W. (2020). Uchanganuzi wa Maudhui na Wahusika Kibibliotherapia katika Hadithi Fupi Teule za Kiswahili. *Editon Cons. J. Kiswahili,* 2(1), 61-75.

---------------------------------------------------------------***---------------------------------------------------------------



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 26.05.2020; Accepted 28.05.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

## Utangulizi

Katika karne hii ya ishirini na moja, bibliotherapia imeanza kutumiwa kwa wingi na wanafasihi kama njia ya kuwaelekeza wanajamii namna ya kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazowakumba maishani. Bibliotherapia ni mbinu ya kusoma vitabu ili kutumika kama kitulizo cha moyo kutokana na hali mbali mbali zinazowakumba wanajamii katika kipindi fulani cha maisha yao. Bibliotherapia ni dhana iliyo na misingi yake katika taaluma ya Sayansi ya Maktaba (Taft, Hotchkiss & Daesik, 2016). Katika bibliotherapia, wasomaji hujihusisha na kusoma, kuhoji na kujadili masuala ambayo wamekutana nayo katika maandishi (Pehrsson & McMillen, 2010). Baadhi ya malighafi muhimu katika bibliotherapia huwa ni fasihi (Graethouse, 2017). Bibliotherapia inaweza kuwasaidia vijana kujielewa na kupambana na matatizo wanayoyapata hasa kupitia fasihi lengwa. Kwa maoni ya Greathouse (2017) hii ni harakati ya mwingiliano wenye nguvu kati ya hulka ya msomaji na fasihi chini ya uelekezo wa mtaalamu au mtu aliye na ujuzi fulani kama vile mwalimu.

Kwa mujibu wa Prater na wenzake (2005) walimu wanaweza kuwasaidia watoto au vijana kutumia bibliotherapia kupitia viwango vitatu ambavyo ni: utambulisho, mtakaso-hisia na umaizi. Utambulisho unadhihirika pale msomaji anapojitambulisha na wahusika au hali fulani katika kazi ya fasihi. Utakaso-hisia unatokea pale msomaji anaposhiriki katika fikra na hisia za mhusika. Umaizi hubainika pale msomaji anapotambua kwamba anahusiana na mhusika au hali fulani na anajifunza namna ya kukabiliana vilivyo na hali tata za maisha yao. Cleveland (2008) anaongeza kiwango cha nne ambacho ni cha ubia. Hiki ni kiwango ambacho mtoto au kijana huweza kutambua kuwa binadamu ulimwenguni kote hupitia katika hali mbalimbali za kimaisha.

**Mapitio ya Maandishi**

Bibliotherapia (BB) ni utaratibu amilifu unaohusu mengi zaidi ya kusoma tu kitabu maalum kwa mwanafunzi (Aiex, 1982). Kulingana na Gardner (1982), hatua ya kwanza katika mchakato wa BB ni 'kujitambua'. Huu ni wakati mwalimu anamuuliza mwanafunzi maswali yanayohusiana na wahusika katika kitabu au matukio na mawazo yaliyomo hadithini. Hatua ya pili baada ya kujitambua ni 'kujifungua". Huu ni wakati ambapo hisia za mwanafunzi zinafungamana na hadithi na anaweza kuweka huru hisia hizo. Hatua ya mwisho ni majadiliano. Hatua hii inamruhusu msomaji kumsaidia mwanafunzi kuelewa tabia na hisia zake na kupendekeza njia mwafaka ya kushughulikia. Majadiliano hayo yanawasaidia wanafunzi kuelewa siyo tu hisia zao binafsi bali pia kujua kwamba hawako peke yao. Kulingana na Aiex (1997), usomaji wa vitabu vya hadithi kwa mwanafunzi humfanya aone kwamba wahusika wengine wanakabiliana na matatizo sawa na yake na kwamba ni njia moja ya kuainisha majadiliano kuhusu matatizo ambayo mwanafunzi angesitasita kujadili. Hali hii inamsaidia kuweka huru shinikizo la hisia zinazojengeka ndani yake.

Natalie (2010), alichunguza ufaafu wa BB akitumia ngano za *Zhuang Zi* na wanafunzi ambao walikuwa na mfadhaiko shuleni. Alitaka kuona ikiwa hizo ngano zinaweza kuwasaidia wanafunzi hawa kupunguza mfadhaiko wao. Masuala yaliyojitokeza katika ngano hizi ni kama vile uhaba wa fedha, kazi za kimasomo zinazochosha za pale chuoni na uhusiano miongoni mwao. Matokeo yalionyesha kuwa wanafunzi wa kike walifaidika sana kupitia zile ngano. Utafiti huu ni tofauti na wetu ambao ulilenga kuchanganua maudhui na uhusika kwa misingi ya BB katika diwani teule za hadithi fupi za Kiswahili. Maudhui yalilengwa ili kubaini ikiwa yanaweza kuwafunza wanafunzi maadili shuleni.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 26.05.2020; Accepted 28.05.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Amer (1999), amependekeza kuanzisha majadiliano ili wanafunzi waweze kushirikisha vitabu vya bibliotherapia katika maisha yao ndani au nje ya darasa. Sullivan and Strang (2002), wanasisitiza kushirikishwa kwa wazazi kwa kuwatumia nakala za baadhi ya kazi, majarida au mazoezi ambayo watoto wao wamemaliza. Walimu wanaweza kuhakikisha kuwa bibliotherapia inaendelea hata nyumbani kwa kuwapa wazazi fununu ya kazi za kusomwa na shughuli ambazo watoto wao wanaweza kufanya wakiwa nyumbani. Mwalimu akiwa darasani anafaa kuteua matini yenye ufaafu zaidi kushughulikia hali fulani ya mtoto au watoto wote.

**Nadharia ya Mapatano ya Mwitikio wa Msomaji (NMMM)**

Kazi hii ilitumia Nadharia ya Mapatano ya Mwitikio wa Msomaji (NMMM) yake Rosenblatt (1995). Nadharia hii imetokana na ile ya mwitikio wa msomaji (NMM). Mwitikio ni mwendelezo wa ushirikiano baina ya mtu binafsi na kazi ya fasihi, ushirikiano huu unaweza kuendelea kwa muda hata baada ya mtu kumaliza kukisoma kitabu. Atwood, (1982), anakubaliana na haya anaposema kuwa kitendo cha usomaji ni mfanyiko unaombadilisha msomaji na hawezi kuwa mtu yule aliyekuwa kabla na baada ya kuisoma matini.

Kazi hii ilijikita katika nadharia ya NMMM kwa sababu hailengi fasihi kivyake lakini pia wasomaji au hadhira inavyoitikia kazi ya fasihi. Walimu wa fasihi ya Kiswahili pamoja na wanafunzi wao walihusishwa katika kuzisoma HF teule za Kiswahili na kuzichanganua ili tuone wanavyoitikia kazi hizi baada ya kuzisoma. NMMM ilibuniwa kwa upana katika eneo la tajriba ya fasihi ya watu wazima. Kwa jumla, nadharia hii inajihusisha na uhusiano kati ya matini na msomaji (Cuddon, 1991) pamoja na msisitizo juu ya njia mbalimbali ambazo msomaji anashiriki wakati anaposoma matini na mitazamo tofauti inayotokea katika uhusiano huo. Matini haiwezi kujitosheleza mpaka msomaji aisome kisha aifasiri (Kennedy, 2010). Mwandishi Paterson (1997) anasema kuwa hadithi nzuri huwa hai, kubadilika na kukua inaposomwa na msomaji. NMMM inajihusisha na michango ya msomaji wa matini.

Rosenblatt (1978) amegawa miitikio ya msomaji katika vitengo viwili ; Kwanza ,kuna mwitikio wa kiujumi ambapo msomaji anaposoma matini huleta tajriba na hisia zake anapoifasiri. Pili, kuna mwitikio wa kieferenti, ambapo inasisitiza ufahamu wa habari asilia. Lengo kuu huwa ni ule ujumbe unazungumziwa katika matini. Mtafiti katika utafiti huu aliegemea miitikio yote miwili ambayo iliwafaa walimu na wanafunzi walipozisoma hadithi fupi teule. Nadharia hii inapendekeza kuwa mtunzi anajenga uhusiano na msomaji ili aweze kugundua maana ya matini (Chambers, 1990). Kwa hivyo asili ya fasihi inafaa kutazamwa kama sanaa ya kutendwa ambapo kila msomaji anajenga utendaji wake wa kipekee unaohusiana na matini. Hii ni kwa sababu wasomaji wote wanaleta hisia, mahangaiko, tajriba zao kuhusu maisha na maarifa yao katika usomaji wao, hivyo kila fasiri ina upekee wake. Msomaji anapoisoma kazi yoyote ile mara ya kwanza hupata maana fulani na anapoirudia kazi hiyo hiyo huenda akapata maana tofauti. Kwa mfano watu wengi wanaposoma kifungu katika Biblia mara ya kwanza huenda wakapata maana fulani, lakini wakirudia kifungu kile kile huenda fasiri ikawa tofauti. Hivyo msomaji ni wakala hai katika uvumbuzi wa maana.

NMMM imejikita katika mihimili ifuatayo, ambayo ilitumika katika utafiti wetu;

i. Nafasi ya msomaji haiwezi kuachwa katika ufahamu wetu wa fasihi. Yeye huwa ni wakala hai anaposoma na hawezi kupuuzwa.
ii. Wasomaji hawatumii maana wanavyowasilishiwa bali wanaunda maana wanavyopata katika fasihi.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 26.05.2020; Accepted 28.05.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

iii. Msomaji huandika matini upya anaposoma kwa kutoa fasiri yake
iv. Hadhira hubashiri na kuyahusisha wayakutayo katika hadithi na yale aliyoshuhudia maishani.
v. Usomaji ni mfanyiko na humbadilisha msomaji.
vi. Msomaji huja na dhana, amali na imani ambazo huthibitishwa na yale anayokutana nayo katika kazi ya fasihi.

Nadharia ya Mapatano ya Mwitikio wa Msomaji ya Rosenblatt (1995) inadai kuwa msomaji na matini lazima washirikiane ili kupata maana. Anaonelea kuwa matini haiwezi kusemekana kuwa na maana bila ya uhusiano wake na msomaji wake. Rosenblatt (1978), anaona msomaji na matini kama washirika katika mfumo wa kufasiri. Anaendelea kusema kuwa kuna usemezano kati ya msomaji, matini na ushairi. Anatumia istilahi mapatano kurejelea michango ya msomaji na matini. Msomaji na matini huwa katika ushirika mkuu. Kulingana na Rosenblatt matini ni kama kichocheo cha kuibua tajriba mbalimbali za zamani, fikira na mawazo kutoka kwa msomaji. Corcoran na mwenzake (1987) wanadai kuwa msomaji anaposoma matini huiandika upya.

NMMM inaweza kutumika darasani ambapo wanafunzi wanaingiliana na matini na kuziona nafasi zao kama wasomaji. Kupitia mkabala huu wanafunzi wanaweza kujifunza kujenga maana zao wenyewe kwa kuhusisha matini na maisha yao wenyewe na kueleza wanayopitia, wanaposoma badala ya kutegemea mwalimu kuifasiri matini hiyo. Kwa kufanya hivyo wanafunzi katika darasa la nadharia hii wanakua wanafunzi hai kwa sababu majibu yao binafsi yanadhaminiwa. Msomaji hana nafasi tuli kama alivyofikiriwa kidesturi bali ni wakala hai katika uvumbuzi wa maana. Mazingara ambayo mwalimu anaunda pale darasani na falsafa yake huchangia mtazamo wa wanafunzi kuhusu fasihi (Karnowski, 1997).

Nadharia ya Rosenblatt inaunga mkono wazo kwamba kuna ushrikiano wa kiakili kati ya msomaji na kile anachosoma. Ni katika mfumo huu wa kiakili ndipo maana inatokea. Anaeleza kwamba tunapofunza fasihi tunalenga namna wanafunzi wanavyojifunza kupata maana katika ishara mbalimbali za matini.Tunashughulikia kuwajuza wanafunzi licha ya ujuzi mdogo walionao au kuchanganyikiwa kwao, kama sehemu ya ukuaji wa maisha yao wanapojaribu kutumia maswala yao na kuyaweka pamoja. Kwa kuwaongoza wanafunzi kusoma, mwelekezi atagundua njia mpya za kufikiri kuhusu mambo ya dunia na hata kuwahusu wenyewe. Bibliotherapia italeta maana ikitumika kwa msingi huu. Wanatherapia na washauri wanahitajika kuelekeza na kufuatilia maana ambazo mtoto anabuni kutoka kwa maneno na ishara mbalimbali kwenye ukurasa fulani. Bibliotherapia ikitumika vizuri inawasaidia wanafunzi kueleza maana wanazobuni kwenye usomaji wa fasihi.

Nadharia hii inasisitiza namna mbalimbali za mwitikio wa msomaji kwa kazi ya sanaa. Inashirikishwa na msomaji, mfumo wa usomaji na mwitikio. Mwanafunzi katika hali hii anakuwa mhakiki bora wa kile anachosoma.

### 1. Jinsi Maudhui Yanaangazia Hali Halisi ya Maisha ya Kila Siku

Ufaafu wa masuala ya kimaudhui katika matini ya fasihi yaliyosomwa na wanafunzi kutimiza bibliotherapia uliibua sehemu muhimu ya makala haya. Maudhui yaliyo na sifa za kibibliotherapia huangazia hali halisi ya maisha na matatizo wanafunzi wanayokumbana nayo kila siku. Maudhui yanafaa yaweze kuathiri mienendo ya wanafunzi na kubadilisha mitazamo yao ya kimaisha kama wanafunzi. Maudhui yanayoangazia hali halisi katika jamii huwa na sifa za kibiliotherapia kwa sababu wanafunzi wanaweza kujihusisha nayo. Masuala haya yamejadiliwa kupitia kundi lengani (FGD). Alama



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 26.05.2020; Accepted 28.05.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

zifuatazo zimetumika **(Mwl**) mwalimu na (**Msh** ) mshiriki ambaye ni mwanafunzi.

**i) Umasikini**

Umasikini unajitokeza katika hadithi hizi fupi na unasawiri hali halisi katika jamii ya wanafunzi na mengine katika mazoea yao. Katika hadithi ya **Ndoto ya Mashaka** umasikini unaangaziwa katika mtaa duni wa Tandale. Wenyeji wa mtaa huu hufanya kazi duni ili kujikimu katika maisha ya kila siku.Wengi hufanya biashara ndogo ndogo. Hii ni hali halisi katika makazi ya mabanda duni. Baadhi ya wanafunzi ni wakazi wa maeneo haya. Uharibifu wa mazingira umekithiri katika makazi haya ya Tandale. Wakazi hutupa taka kila mahala. Hawatunzi mazingira yao. Mrundo wa taka umetapakaa kila mahala. Hii ni hatari inaweza kusababisha magonjwa, hata maji yanayotumiwa humwagwa katika mto Msimbazi. Baadhi ya wanakikundi walikubaliana na haya;

**Msh 7:** *Hali ya umasikini ni sehemu ya maisha ya wanafunzi wengi. Kuna baadhi huishi katika vitongoji duni. Wanafunzi katika vitongoji duni huchangia uharibifu wa mazingira. Taka hutupwa ovyo njiani.Uharibifu wa mazingira. Katika mtaa duni wa Tandale kuna mrundo wa taka. Maji yanayotumiwa humwagwa katika mto Msimbazi.*

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Kauli za wanakikundi zinathibitisha kuwa maudhui yanayojitokeza katika hadithi hizi fupi yanasawiri hali halisi katika jamii ya wanafunzi na mengine katika mazoea yao. Mapenzi shuleni vile vile yanazungumziwa.

**ii) Mapenzi shuleni**

Wanafunzi wengi shuleni na hasa katika shule za upili wana mazoea yakujihusisha katika mapenzi. Hii huwa ni hatari kwao kwani wale wanafunzi wakike huishia kuwa wajawazito na kuishia kukomesha masomo yao. Katika hadithi za **Kanda la Usufi,** na **Shogake dada ana ndevu** maudhui ya mapenzi shuleni yanaangaza hali halisi ya maisha ya kila siku ya wanafunzi. Sela na Masazu wanajiingiza katika uhusiano wa kimapenzi wakiwa shuleni na matokeo yake ni kuwa Sela anapata mimba asiyotarajia na kuathirika pakubwa kimasomo. Mimba hiyo ilizua mgogoro kati ya Sela, mamake na babake mzee Butali. Naye Safia anawahadaa wazazi wake mwishowe anaavya mimba hili jambo linasababisha kifo chake. Anakubaliana na wazazi kumwalika Kimwana nyumbani amsaidie kudurusu vitabu. Kimwana hufika pale akiwa amejifunika buibui mwili wote. Safia baada ya muda anakuwa mjamzito. Lulua kakake Safia anagundua kuwa Kimwana ni mwanamume ila aliwahadaa kwa kujifunika buibui. Huu ni uhalisia uliopo katika jamii. Uavyaji mimba ni tendo linalotokea kwa wanafunzi wengi Wanakikundi wanakubaliana na haya katika mazungumzo yao;

**Msh 2:** *Maudhui katika* ***Kanda la Usufi*** *yanaangazia hali halisi katika maisha ya wanafunzi. Mapenzi shuleni mara nyingi huwa ni mapenzi bandia. Sela alipata mimba na kuacha masomo, ndivyo wanafunzi wanaacha masomo kwa sababu ya mimba zisizohitajika.*

(Chanzo:Data ya nyanjani)



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 26.05.2020; Accepted 28.05.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Mapenzi shuleni husababisha mimba za mapema ambazo hutokea wanafunzi wangali shuleni. Hii ni hali halisi katika jamii na hasa kwa wanfunzi shuleni. Hata wale wa shule za msingi wamethiriwa na hili. Mimba za mapema huwa ni kero kwa watoto wa shule ambao hudanganyika kwa kuavya hivyo kuhatarisha maisha yao na hata kuishia kuaga dunia.

**iii) Dawa za kulevya**

Matumizi ya dawa za kulevya yana athari zake kwa familia na jamii . Watu wengi wameathirika na janga hili, jinsia zote wanawake kwa wanaume. Katika shule za upili idadi ya wanaoshiriki dawa hizi ni nyingi. Maudhui ya dawa za kulevya katika hadithi fupi **Fumbo la Mwana** yanaathiri wanafunzi moja kwa moja. Wanashiriki matumizi mabaya ya dawa za kulevya shuleni. Nanda ambaye ni mwanfunzi wa shule ya upili anaanza kutumia dawa za kulevya. Akarudi nyuma kimasomo na kiafya akaacha hata kuoga. Katika hadithi fupi ya **Gilasi ya Mwisho Makaburini,** wahusika Msoi na Asha wanaingilia matumzi ya dawa za kulevya. Tatizo la dawa za kulevya limekuwa donda sugu kwa serikali. Kwa mfano,

**Msh 4:** *Bw. Makulu alianza kumhusisha Nanda katika uuzaji wa dawa za kulevya.*
*Akaanza pia kuzitumia. Akarudi nyuma kimasomo na kiafya akaacha hata kuoga.*
*Ikabidi walimu kumuita mzazi wake.*

(Chanzo:Data ya nyanjani)

Kauli za wanakundi zinathibitisha kuwa dawa za kulevya huathiri wanafunzi moja kwa moja. Hii ni hali halisi katika jamii. Huwaathiri vijana wa shuleni na vyuoni pakubwa. Uraibu huu huwaathiri wanafunzi kimasomo na kiafya. Mhusika Nanda anaathirika pakubwa katika mazingira ya shuleni na hata nyumbani.

**iv) Ndoa za lazima/mapema**

Katika jamii nyingi za Kiafrika wanafunzi wakike huathiriwa na maswala ya ndoa za mapema na za lazima. Katika hadithi fupi ya **Ngome ya Nafsi,** maudhui yanayoangazwa ni ya hali halisi katika jamii kuna ndoa za mapema na za lazima. Wazazi kama vile mzee Mengo wana na tamaa ya kupata mali. Katika hadithi fupi ya **Kijembe cha Ngariba** mwandishi anamulika suala la tohara kwa watoto wakike. Hii ni hali halisi katika jamii zenye tamaduni potovu kama hizi. Wazee kuthamini mahari kuliko masomo ya mabinti zao. Wasichana wengine hupoteza maisha yao baada ya kuvuja damu nyingi. Rafikiye Rita ambaye ni Clara anatoroka kupashwa tohara. Baadhi ya wanakikundi wanadai;

**Msh 5:** *Mzee Mengo haoni haja ya kusoma kwa mtoto wakike anachohitaji ni*
*mahari. Mamake Naseko hana la kusema. Msichana Naseko anatorokea kwa makao*
*ya wototo wakike kwa Bi. Tesi. Anapitia msituni na kwenye giza totoro.*

(Chanzo: Data ya nyanjani)

Tamaduni potovu katika jamii huwanyima wasichana nafsi ya kusoma badala yake wakiozwa ili wazazi walipwe mahari. Tamaduni hizi husababisha ndoa za lazima na mapema. Katika hadithi ya **Kipenda Moyo ni Dawa** Nandako ni mwanafunzi aliyekuwa ameufanya mtihani wa kidato cha nne alikuwa akisubiri matokeo ya mtihani huo Anaamua kuolewa kwa mzee Fwamba na kukataa kujiunga na chuo kikuu. Hii ni ndoa ya mapema.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 26.05.2020; Accepted 28.05.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Wanafunzi kukosa kufanya maamuzi ya busara. Nandako kuamua kuolewa na mzee Fwamba badala ya kujiunga na chuo kikuu baada ya kupata alama A. Kuna maudhui ya uhuni ambapo wanaoendesha pikipiki kuwachezea wanafunzi wa shule kama Nandako. Tunamwona akisumbuliwa pale kituo cha basi kila mmoja akitaka kumbeba. Katika jamii zetu usafiri wa kutumia pikipiki au *bodaboda* umesheni kila pembe nchini. Wateja wao kwa wingi hujumlisha wanafunzi wa shule. Hawa waendeshaji pikipiki wana tabia ya kuwachezea wanafunzi wakike. Katika maeneo mengine wao pia huwapachika mimba jambo ambalo hukatiza masomo yao na kusababisha ndoa za mapema na lazima.

Maudhui haya yanaibua taswira halisi katika jamii. Mawazo haya yanalingana na matokeo ya utafiti ya Natalie (2010), aliyegundua kuwa hadithi fupi zilishughulikia maudhui yanayowaathiri vijana kama uhaba wa fedha, kazi za kimasomo zinazochosha za pale chuoni na mahusiano miongoni mwao.

**a) Maadili Kutokana na Maudhui ya Hadithi Fupi Teule**

Uwezo wa hadithi fupi kubadili mtazamo wa mwanafunzi ni kielelezo cha kwanza kuwa hadithi fupi ina athari ya kibibliotherapia kwa msomaji. Chambers (1990) anasisitiza kuwa nadharia hii ya mapatano ya mwitikio wa msomaji (NMMM) inapendekeza kuwa mtunzi anajenga uhusiano na msomaji ili aweze kugundua maana ya matini. Kwa hivyo asili ya fasihi inafaa kutazamwa kama sanaa ya kutendwa ambapo kila msomaji anajenga utendaji wake wa kipekee unaohusiana na matini. Kwa mkabala huu, utafiti ulilenga kuchunguza athari ambazo hadithi fupi zinaweza kuwa nazo kwa mwanafunzi na mtazamo wake. Matokeo yake yamewasilishwa maelezo yafuatayo;

Mapenzi shuleni huleta madhara kwa wanafunzi. Wengine huacha masomo ilihali wengine huavya mimba na kukatiza maisha yao. Katika hadithi za **Kanda la Usufi** na **Shogake Dada ana Ndevu.** Sela na Masazu wanajiingiza katika uhusiano wa kimapenzi wakiwa shuleni na Sela anapata mimba asiyotarajia na kuacha masomo. Wanafunzi wengi hujipata katika hali iliyowakumba Sela na Masazu. Nafasi ya mwanamke inadhihirika wakati mamake Sela analaumiwa na Mzee Butali kuwa hakumwelekeza mtoto wake vyema. Hii ni ishara kuwa katika maisha ya kisasa, wanawake wanaendelea kulaumiwa wakati wasichana wao wanapopata mimba za mapema. Safia naye anawahadaa wazazi wake na kuishia kuavya mimba . Anakubaliana na wazazi kumwalika Kimwana nyumbani amsaidie kudurusu vitabu. Hufika amejifunika buibui mwili wote. Uavyaji mimba ni tendo hatari linaweza kusababisha kifo kama ilivyotokea kwa Safia. Ni funzo hasa kwa wanafunzi wa kike.Haya yanathibitishwa na wanafunzi hawa wasemapo;

**Msh 3:** *Ni muhimu kutia bidii masomoni kama alivyofanya Safia. Alitia bidii masomoni.*

*Uavyaji mimba ni hatari vijana wengi hupoteza maisha yao kama ilivyokuwa kwa Safia.Vijana wanasawiriwa kuwa waongo. Safia anawadanganya wazazi anadurusu kujiandaa kwa mtihani ilihali anazini na Kimwana. Vijana wajiepushe na uongo.*

Katika hadithi fupi ya ***Gilasi ya Mwisho Makaburini*** katika diwani ya ***Damu Nyeusi na hadithi nyingine*** wahusika Msoi na Asha wanaingilia matumzi ya dawa za kulevya.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 26.05.2020; Accepted 28.05.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Siku moja wanaenda makaburini wanakutana na wezi ambao wanawavamia na kuwapora. Ulevi na anasa kama maudhui yanajitokeza. Vijana wanajihusisha katika mapenzi. Mhusika Msoi anabadilisha nia na anaacha kwenda makaburini. Funzo kuu hapa kwa vijana ni kujiepusha na matumizi ya dawa za kulevya na mapenzi ya kiholela. Kauli ya **Msh 3** inathibitisha:

**Msh 3:** *Dawa za kulevya zinaweza kudhuru afya ya mtu yeyote. Maisha kuharibika na wanafunzi kurudi nyuma kimasomo kama ilivyokuwa kwa Nanda.*

Ni muhimu kutia bidii masomoni kama alivyofanya Safia. Alitia bidii masomoni. Uavyaji mimba ni hatari vijana wengi hupoteza maisha yao kama ilivyokuwa kwa Safia.Vijana wanasawiriwa kuwa waongo. Safia anawadanganya wazazi anadurusu kujiandaa kwa mtihani anapomwalika Kimwana nyumbani kwao. Mwishowe Safia anapata mimba.Vijana wajiepushe na uongo. Mwishowe Safia kukosa kuendelea na masomo yake. Haya mafunzo ni muhimu kwa wanafunzi wote. Wazingatie masomo na wajiepushe mapenzi wakiwa shuleni na uavyaji mimba ni hatari huenda ukapoteza maisha yako.

**Msh 5**: *Shogaake mwenye ndevu alikuwa ni mvulana Kimwana. Mwishowe Safia anapata mimba na kukosa kuendelea na masomo yake. Haya ni Mafunzo muhimu kwa wanafunzi wote.*

Uzembe shuleni husababisha kufeli mtihani kama ilivyo kwa Samuel katika hadithi ya **Mtihani wa Maisha.** Wanafunzi kupata funzo kuwa kuanguka mtihani sio mwisho wa maisha. Baada ya kuanguka mtihani suluhu si kujiondoa uhai. Kutaka kujiondoa uhai kama anavyofanya Samuel kujitosa majini ili afe hakufai .Wanakijiji kwa ushirikiano wanamwokoa.

**Msh 1**: *Hakuna haja ya kujitoa uhai baada ya kuanguka mtihani. Huo si mwisho wa maisha.*

Wanafunzi wanajifunza kuwa na msimamo thabiti kama Naseko. Katika hadithi ya **Ngome ya Nafsi** anayetoroka ndoa ya lazima na mapema na badala yake kurudi shuleni kusoma**.** Nafasi ya mwanamke si jikoni anaweza kujikimu kupitia kisomo au elimu. Kuna mashirika ya kuwasaidia watoto wakike wanaopitia hali hizo. Naseko anatorokea kwa Bi. Tesi. Katika hadithi fupi ya **Kijembe cha Ngariba** watoto wakike kulazimishiwa tohara. Wazee kuthamini mahari kuliko masomo ya mabinti zao. rafikiye Rita ambaye ni Clara anatoroka kupashwa tohara. Wanafunzi wawe kama Clara kutafuta usaidizi mila potovu zinapolazimishwa na wazazi. Anapata shirika linalomtorosha hadi ng'ambo.

***Msh 1:*** *Wanafunzi kuwa na msimamo thabiti kama Naseko anayetoroka ndoa ya lazima na mapema na badala yake kurudi shuleni kusoma.Clara naye kutoroka kijembe cha ngariba ili aendeleza masomo badala ya kuozwa.*

Mifano hii inaonyesha kuwa wanafunzi hujifunza mengi kupitia hadithi fupi teule.

Mafunzo haya yanakuwa ni chanzo cha kutagusana na wahusika katika hadithi hizo. Kulingana na Aiex (1997), usomaji wa vitabu vya hadithi kwa mwanafunzi humfanya aone kwamba wahusika wengine wanakabiliana na matatizo sawa na yake. Huu ndio mwanzo wa bibliotherapia pale darasani. Wanafunzi walifundishwa mafunzo ya kujiepusha na mihadarati na anasa. Uavyaji mimba ni hatari wanapaswa kuwa na msimamo thabiti kama Clara na Naseko kupinga



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 26.05.2020; Accepted 28.05.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

tamaduni potovu.. Mapenzi ya shuleni hayana faida nan i vyema kujiepusha na migomo shuleni. Utunzaji wa mazingira unatiliwa maanani. Vijana wanastahili kuwa viongozi waliowajibika. Vijana wanahitaji kukuza maadili katika jamii.

### b) Jinsi Maudhui Yanamsaidia Mwanafunzi Kutatua Matatizo Yake

Utafiti huu ulilenga kupeleleza sifa za kibibliotherapia za hadithi fupi. Hivyo basi, utafiti ulitaka kubaini nafasi ya maudhui katika hadithi fupi katika kusaidia wanafunzi kutatua matatizo wanayokumbana nayo kibinafsi. Sehemu hii ilishughulikia suala hili pamoja na majibu ya wanafunzi kuhusu uwezekano wa wanafunzi kusuluhisha changamoto zao kwa kutumia maudhui waliyopitia katika hadithi fupi zifuatazo:

Katika hadithi ya **Kanda la Usufi** maudhui ya mapenzi shuleni yanamsaidia mwanafunzi kujua madhara yake. Hivyo basi, anajitahadharisha dhidi ya kujihusisha na mapenzi shuleni. Katika maudhui ya nafasi ya mwanamke, mtu anajifunza kuwa si mama pekee anafaa kuulizwa kuhusu upotovu wa nidhamu ya mtoto msichana. Baba pia huwa na jukumu la kuwapa maadili watoto wao. Njia ya kutatua tatizo hili la wanawake kuonekana kama ambao hawaelekezi wasichana wao, ni kuwa wasichana wawe na nidhamu na waachane na mapenzi ambayo huleta mimba za mapema.

Katika hadithi ya **Shogaake ana Ndevu** mwanafunzi wakike anaweza kutatua tatizo lake hasa ikiwa ana uhusiano na vijana wakiume atajihadhari na kuacha huo urafiki ili aendeleze masomo yake. Na ikiwa ni mjamzito atajiepusha kuavya mimba kwani ni hatari. Huenda akapoteza maisha yake alivyofanya Safia. Katika hadithi ya **Ngome ya Nafsi** na **Kijembe cha Ngariba** jamii ambazo watoto wakike wanaozwa mapema hadithi hii itasaidia hasa kumuiga Naseko na Clara. Hawa wawili wanapinga tamaduni potovu katika jamii zinazolazimisha ndoa za mapema na lazima. Wanachukua hatua ya kutoroka ili waweze kuendelea na masomo yao. Watoto wakike wasidharauliwe kwamba mahala pao ni jikoni. Wanafunzi Kujifunza kuwa na msimamo thabiti kama Clara na Naseko.

Katika hadithi ya **Kipenda Moyo ni Dawa** wanafunzi hujifunza kufany maamuzi mwafaka maishani mwao. Mhusika Nandako anaamua kuolewa na mzee Fwamba badala ya kwenda Chuo Kikuu baada ya kupita mtihani wa kidato cha nne. Huu ulikuwa uamuzi usiofaa. Wanafunzi wengi huishia kufanya maamuzi ambayo hayawasadii maishani. Wengine hutoroka shuleni ili kwenda kuolewa. Pili bidii masomoni huzaa matunda Nandako anapata alama ya A baada ya kufanya bidii shuleni. Ndoa za mapema hukatiza masomo jinsi masomo ya Nandako yanavyokatizwa. Matokeo haya yanashadidia anayosema Atwood (1982) akisisitiza dhima ya NMMM, anaposema kuwa kitendo cha usomaji ni mfanyiko unaombadilisha msomaji na hawezi kuwa mtu yule aliyekuwa kabla na baada ya kuisoma matini. NMMM ina ile nadharia ya mapatano ya mwitikio wa msomaji ya (Rosenblatt, 1995).

Mijadala ya kundi lengani inaonyesha kwamba hadithi fupi zinazosomwa darasani ni za kuaminika na maudhui yanaeleweka vizuri na wanafunzi. Maudhui haya hujitokeza katika hali halisi ya maisha na hushughulikia masuala ya kijamii,kiuchumi na kielimu. Maudhui haya huwasaidia kwa kiasi kidogo kutatua matatizo ya kijamii lakini hata hivyo hufunza maadili. Matokeo haya ni muhimu kwa dhana ya bibliotherapia kama inavyotafitiwa katika utafiti huu. Ufaafu wa maudhui kwa mahitaji ya wanafunzi ni muhimu ili faida za kibibliotherapia zipatikane. Hata hivyo, matokeo kwamba



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 26.05.2020; Accepted 28.05.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

maudhui yanashughulikia masuala ya kijamii kwa kiasi kidogo yanatilia shaka ufaafu wa maudhui kama chombo cha kufanikisha bibliotherapia kupitia ufunzaji wa hadithi fupi katika shule za upili. Zaidi ya hayo, wanafunzi walitaja kwamba yanashughulikia maadili kwa kiasi kikubwa jambo linaonyesha umuhimu ambao wanafunzi wanatilia maudhui hayo.

**2. Wahusika Katika Hadithi fupi Wanapitia Matatizo Yapi?**

Baada ya kuchunguza maudhui, utafiti uliendelea kuchunguza athari za wahusika wa hadithi kwa wasomaji. Wahusika pia wana umuhimu kwa sababu wanakumbana na kusuluhisha changamoto kwa njia mbalimbali ambazo wasomaji wanaweza kuiga. Kulingana na Aiex (1997), usomaji wa vitabu vya hadithi kwa mwanafunzi humfanya aone kwamba wahusika wengine wanakabiliana na matatizo sawa na yake ni njia moja ya kuainisha majadiliano kuhusu matatizo ambayo mwanafunzi angesitasita kujadili. Hali hii inamsaidia kuweka huru shinikizo la hisia zinazojengeka ndani yake. Kwa mtazamo huu , utafiti ulilenga kubaini sifa za kibibliotherapia katika wahusika wa hadithi fupi teule katika utafiti huu. Wahusika walio na sifa hizi wanafaa kuaminika katika hali halisi ya maisha na kukabiliana na matatizo ya kijamii na kielimu. Wahusika wanastahili kufunza maadili kwa wanafunzi na waweze kuwasaidia kubadili mitazamo yao kimaisha. Majibu ya wanafunzi yameonyeshwa baada ya kuzisoma hadithi fupi hizi katika maelezo yafuatayo;

Wahusika katika hizi hadithi fupi teule hupitia matatizo aina mbali mbali. Katika hadithi ya **Kanda la Usufi** wahusika Sela na Masazu wanashiriki mapenzi wakiwa shuleni. Sela anapata mimba na inambidi kuacha masomo. Hawa wote ni wanafunzi hawana pesa za kumtunza mwanao. Kauli za hawa wanafunzi zinathibitisha haya;

**Msh 2:** *Sela na Masazu pia wanafukuzwa shuleni baada ya Sela kupata mimba . Wazazi wa Sela pia ni masikini kwani hawampi mtoto wa Sela malezi bora yanayohitajika. Kupata mimba kwa Sela pia kunazua mzozo kati ya mzee Butali na mkewe. Mzee Butali anamfukuza mkewe na bintiye nyumbani kwa kumlaumu kuwa hakumwelekeza bintiye vyema.*

Mhusika Sela kwa sababu ya kujihusisha na mapenzi shuleni inasababisha yeye kupata mimba kisha kufukuzwa shuleni. Nyumbani Mzee Butali babake Sela anamlaumu mamake na kisha anawafukuza kutoka nyumbani. Umasikini pia ni tatizo kwake Sela kwani hawezi kumtunza mwanawe baada ya kujifungua. Masazu naye pia hana kazi.

Katika hadithi fupi ya **Fumbo la Mwana** familia ya mhusika Nanda ni masikini wanamtegemea mzee Makulu. Huyu mzee humpatia kazi dukani na shambani. Baadaye Nanda anabadilika kitabia hata pale shuleni. Atanas babake Nanda kuhuzunika kwa sababu ya kubadilika kwa tabia ya Nanda. Mzee Makulu anawatumia Nanda na vijana wengine kumuuzia bangi na anawashawishi kuivuta. Tabia ya Nanda inadorora na walimu wanagundua haya. Haya yanaangaziwa na wanafunzi wafuatao;

**Msh 6**: *Nanda alifika shuleni kuchelewa. Ni mlegevu na mchafu.*

**Msh 8:** *Kimasomo anarudi nyuma na kukosa viwango vya usafi*

Nanda kuanza kuvuta bangi. Dawa za kulevya ni hatari. Matatizo yanakuwa mengi kwake



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 26.05.2020; Accepted 28.05.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Darasani anarudi nyuma kimasomo. Haogi ni mchafu hazingatii viwango vya uchafu. Walimu kulalamikia tabia yake na kumwalika babaka mzee Atanas kufika pale shuleni ili kuzungumzia suala hili.

Naseko katika hadithi ya **Ngome ya Nafsi** kunyimwa nafasi ya kuendelea na masomo na babake ameshapokea mahari kutoka kwa mzee Sakaja. Naseko kubebwa na kupelekwa kwa mumewe mzee Sakaja lakini anamua kutoroka usiku. Anatorokea kwa Bi Tesi makao ya watoto ili apate nafasi ya kuendelea na masomo yake. Mamake Naseko kulazimishwa kunyamaza hata ikiwa hakubaliani na ndoa za lazima.

**Msh 4:** *Naseko kuozwa kwa mzee Sakaja.kwa sababu babake alikuwa kapokea mahari. Hakuthamimi elimu ya mtoto msichana*

Naseko analazimishiwa ndoa ya lazima na mapema. Anaozwa kwa mzee Sakaja ambaye alikuwa tayari na wake wengine. Babake Naseko kushikilia tamaduni zilizopitwa na wakati.
Naseko kwa sababu ya msimamo wake thabiti anatoroka kwa mzee Sakaja usiku wa manane na kupitia msituni ili afike kwa Bi Tesi.

**a) Jinsi Wahusika Wanatatua Matatizo Yao**

Utafiti pia ulilenga kubaini iwapo wahusika waliweza kutatua migogoro wanayokumbana nayo katika hadithi. Dhana hii ya utafiti iliegemea mtazamo kwamba bibliotherapia inatokea kupitia kuhusisha mapitio ya msomaji na yale ya wahusika. Wanafunzi shuleni wanapotagusana na wahusika katika hadithi wanafaa kuiga jinsi wanavyotatua matatizo yao. Mawazo haya yanasisitizwa na Abdullah (2002) anaposema, ikiwa mtoto au kijana hawezi kuwa na mtagusano na mhusika inawezekana kwamba fasihi iliyochaguliwa haifai au labda, mtoto anahitaji vitu kadhaa halisi ili kuifanya hadithi kuwa ya kweli kwao. Matokeo kuhusu suala hili yametolewa katika vielelezo vifuatavyo:

Katika hadithi fupi ya **Kanda la Usufi** mgogoro uliokuwepo kati ya Mzee Butali na mkewe ambapo alikuwa akimlaumu mkewe kuwa chanzo cha bintiye Sela kupata mimba na kufukuzwa shuleni kwa sababu hakumuelekeza. Anaamua kumfukuza mkewe na bintiye Sela kutoka nyumbani. Mzozo huu ulitatuliwa na wanajamii na hivyo basi Mzee Butali akawaita kurudi kwake. Wanapanga safari yao usiku na mvua ilikuwa nyingi Sela akiwa amembeba mtoto anateleza na kuanguka mtoni. Anaaga dunia. Walifikiria hilo ni suluhisho badala yake mauti yakatokea. Kupitia Masazu na Sela, tunaona umuhimu wa kuwatii wazazi. Wao hawakuona kuwa wazazi walikuwa wakiwasaidia kumlea mtoto wao kadogo. Walipoenda kuiba mtoto huyo, ndipo Sela na mtoto Kadogo walipatwa na msiba. Kuwatii wazazi kungewasaidia kujiepusha na msiba huo. Mzee Butali licha ya kuwa na hasira na kumfukuza mkewe, aliweza kumsamehe na kumrudisha nyumbani. Kupitia Mzee Butali tunaona kuwa ni vizuri kuwa mtu wa kusamehe.

Naseko katika hadithi ya **Ngome ya Nafsi** ana msimamo thabiti. Babake mzee Mengo anapanga kumuoza Naseko kwa Mzee Sakaja ili apate mali. Hathamini elimu ya mtoto wakike. Mzee Mango ana taasubi ya kiume kwani mamake Naseko haruhusiwi kuzungumza kuhusu jambo la kuozwa kwa binti yao. Naseko anatoroka nyumbani kwake mzee Sakaja na kutafuta usaidizi kwa Bi. Tesi aliye na makao ya watoto. Jambo hili lamwezesha kuendelea na masomo. Clara vile vile katika **Kijembe Cha Ngariba** ana msimamo thabiti anapinga tamaduni hizi zilizopitwa na wakati. Anatoroka tohara ili apate nafasi ya kuendelea na masomo. Tamaduni zilizopitwa na wakati hazifai. Wanafunzi katika mjadala wanatoa maoni yao;


© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 26.05.2020; Accepted 28.05.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

**Msh 3:** *Njia nyingine ni Kushirikiana na walimu shuleni na hata wasimamizi wa dini.*

**Msh 4:** *Wazazi kuhamamishwa kuhusu tamaduni potovu.*

Wahusika hawakutatua matatizo yao wenyewe ila walihitaji jamii kushughulikia changamoto hiyo. Ufichuzi huu unabainisha mchango wa asasi za kijamii katika kutatua matatizo ambayo watu hukumbana nayo. Clara kutoroka tohara kuenda ughaibuni kwa usaidizi wa shirika fulani ili aendeleze kisomo chake. Changamoto za wahusika zinamsaidia msomaji kuepuka kujiingiza katika hali zizo hizo.Wanafunzi hupata mafunzo kupitia maudhui. Wanafunzi wanastahili kuwajibika kwa ili watunze mazingira yao. Hii inabaini namna wanafunzi wanavyowaelewa wahusika na changamoto wanazopitia na jinsi wanafunzi hufasiri changamoto hizo. Udhaifu huu kwa upande wa wanafunzi unaweza kuchangia kukosa kupata faida za bibliotherapia zinazosababishwa na wahusika. Udhaifu huu wa wanafunzi unaonekana kuwa unatokana na maelekezo wanayopewa na walimu. Hata hivyo, walimu walihisi kwamba palikuwa na mafunzo muhimu ambayo wanafunzi wangeweza kujifunza kutokana na mapitio ya wahusika.

Hii yaonyesha mafunzo yanayotokana na mapitio ya wahusika bali sio namna wahusika walivyozitatua changamoto hizo wenyewe. Hii inabainisha nafasi ya walimu ya ushauri kwa jumla na wanachukua nafasi yoyote kutekeleza wajibu huu. Mawazo ya wahusika kuweza kukabiliana na matatizo yao yanahimizwa kama njia moja ya kuwezesha bibliotherapia. (Maich na Kean (2004), wamekuza mwongozo ufuatao kuhusu wahusika;

*Je, wahusika wanaonyesha mbinu za kukabiliana na shida na je, inaonyesha suluhu za matatizo?*

Wanafunzi wanaelezea mafunzo waliyojifunza bali sio mabadiliko ya kimawazo waliyopata kutoka kwa hadithi fupi. Matokeo hayo yanafichua udhaifu wa wanafunzi kuhakiki nafasi za wahusika na athari zao kwa maisha yao. Zaidi ya hayo, uwezo wa wanafunzi wa kufaidika kupitia kujitambulisha na wahusika hivyo basi unatiliwa shaka.

**b) Uaminifu wa Uhalisia wa Wahusika**

Fasihi iliyo na wahusika wenye sifa za kibibliotherapia huwa wanaaminika katika hali halisi ya kijamii. Wahusika hutumiwa katika kazi za fasihi ili kuwakilisha hali halisi katika jamii. Hawa huwa ni wahusika ambao wanafunzi wanaweza kutagusana nao kwa urahisi. Kupitia mjadala wa kundi lengani wanafunzi waliweza kuelezea baadhi ya wahusika katika hadithi fupi teule ambao wanaaminika katika hali halisi katika jamii. Hizi ni baadhi ya kauli za wanafunzi;

**Msh 5:** *Katika hadithi fupi ya* ***Kanda la Usufi*** *Sela na Masazu ni wanafunzi wa shule ya upili. Wanashiriki mapenzi wakiwa shuleni na Sela anakuwa mjamzito na kuzaa mtoto.*

Mapenzi shuleni ni hatari. Wanafunzi wengi huathirika kupitia hili. Wanafunzi wakike huathiriwa pakubwa kupitia kupata mimba za mapema na kuishia kujifungua na au hata wengine kuavya mimba na kuaga dunia.

**Msh 8:** *Nanda katika* ***Fumbo la Mwana*** *ni mwanafunzi wa shule ya upili. Anaanza kushiriki mihadarati shuleni. Athari zinakuwa ni kurudi nyuma kimasomo na kuzorota kiafya.*

Tatizo la ulevi katika jamii limezidi hasa miongoni mwa vijana wa shuleni na vyuoni. Madhara yanayotokana na ulevi huu ni yakiwemo ya kiafya na kuishia kuacha masomo. Maendeleo katika jamii hurudi nyuma kwa kukosa wafanyikazi wenye nguvu ambao ni vijana.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 26.05.2020; Accepted 28.05.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

### c) Maadili kutokana na Wahusika

Wahusika ni viumbe wanaotumiwa na mwandishi kuendeleza dhamira yake. Kwa mujibu wa Wamitila (2008), wahusika ni nyenzo kuu katika fasihi kwa sababu wao ndiyo dira ya matukio na matendo yanayopatikana katika kazi ya kifasihi inayohusika. Kupitia kwa wahusika wasomaji hujifunza maadili. Wahusika wa kifasihi hawahitaji kupendwa kutokana na maadili yao bali wanachotakiwa kufanywa ni kueleweka. Wanafunzi hujifunza mengi kupitia wahusika katika hadithi teule. Kauli za hawa wanafunzi zinajitokeza;

**Msh 7:** *Naseko ana msimamo thabiti anatoroka ndoa ya lazima ili kuendelea na masomo katika* **Ngome ya Nafsi.** *Anapinga tamaduni potovu za ndoa za mapema. Msimamo sawa unachukuliwa na Clara anapotoroka tohara katika* **Kijembe cha Ngariba.** *Wanafunzi wanajifunza kuwa na msimamo thabiti maishani.*

Wanafunzi wanajifunza mengi kupitia hawa wahusika. Hatari ya mapenzi ya shuleni, mimba za mapema, uavyaji mimba na ndoa za lazima. Mifano Zaidi inatolea na wanafunzi;

**Msh 4**: *Mzee Mago katika hadithi ya* ***Tumbo lisilo Shiba*** *ni mfano mzuri wa kuigwa na wanafunzi. Ana msimamo thabiti na ni mtetezi wa kupigania haki za raia Madongo poromoka. Viongozi wana tamaa ya kuwapokonya ardhi yao.*

Mzee Mago ni kielelezo bora kwa wanafunzi. Wanajifunza umuhimu wa kuwatetea raia katika jamii na kutokuwa na tamaa ya kujilimbikia mali huku wakiwadhulumu wenzao.

**Msh 8**: *Biti Kidebe ni mhusika aliye wajibika katika jamii. Ni mfano mzuri wa kuigwa na wanafunzi katika hadithi ya* ***Ndoto ya Mashaka.*** *Tunamuona akimlea Mashaka baada ya wazazi wake kuaga. Anaamua kumpeleka shule ingawa hali ilikuwa ngumu.*

Wanafunzi wakiwa shuleni au vyuoni wanafaa kuzingatia masomo yao badala ya kujiingiza katika uhusiano wa kimapenzi na starehe zisizo na faida. Mwishowa wao hujuta. Hili ni funzo kwa wanafunzi wote.

### Hitimisho

Mjadala wa kundi lengani unaonyesha kuwa wanafunzi walibaini kwamba wahusika wanaaminika katika hali halisi ya kimaisha na wamekabiliana na matatizo ya kibinafsi katika maisha yao. Zaidi ya hayo, wanafunzi wanaweza kujitambulisha na wahusika hawa . Kwa mujibu wa hili suala, wahusika hupitia matatizo ambayo wanafunzi hupitia na huwafunza maadili. Data zaidi zilifichua kwamba wanafunzi waliweza kupata mafunzo kuhusu namna ya kushughulikia matatizo yao wenyewe kupitia kwa wahusika. Matokeo kuhusu wahusika wa hadithi fupi yanaonyesha umuhimu wa wahusika katika kuathiri tabia ya mwanafunzi. Zaidi ya hayo, matokeo yanaonyesha umuhimu wa wahusika katika kufanikisha bibliotherapia kupitia kwa mahusiano na wasomaji. Matokeo hayo ya wanafunzi yanaingiliana na yale ya walimu kuhusu ufaafu wa maudhui na wahusika wa hadithi fupi. Majibu ya wanafunzi yalilengwa sababu mbili. Kwanza ni kubaini uhakika wa walimu kuhusu ufaafu wa maudhui na wahusika wa hadithi fupi kwa mahitaji ya kibinafsi ya wanafunzi; na pili, kubaini maoni ya walimu kuhusu ufaafu wa hadithi fupi wa kufanikisha bibliotherapia kwa wanafunzi. Matokeo haya yanawiana na data za awali za wanafunzi. Matokeo haya yanaonyesha kwamba hadithi fupi za Kiswahili zina uwezo mkubwa wa kufanikisha bibliotherapia kupitia kwa kujinasibisha na maudhui kuliko wahusika katika



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 26.05.2020; Accepted 28.05.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

hadithi hizi. Maarifa pia yanaweza kuelezwa kama hatua ya kufikia hali ya kujitambua na kutumia kazi ya fasihi (msuko, wahusika au mahusiano) kwa maisha yao.

**MAREJELEO**


Abdullah, M. H. (2002). Bibliotherapy. *ERIC Clearinghouse on Reading, English, and Communication Digest #177.*

Aiex, N. (1996). Bibliotherapy. *Learning Disabilities OnLine*. ERIC Digest 82 Retrieved February25, 2017 from http://www.ldonline.org/ld_store/bibliotherapy/eric_digest82.html.

Aiex, N. K. (1982). *Bibliotherapy fact sheet*. Urbana, IL: ERIC Clearing House on Reading and Communication skills. ED. 234338.

Amer, K. (1999) Bibliotherapy using fiction to help children in two populations discuss feelings. Paediatric Nursing, 25(1), 91

Atwood, M. (1982): *Second words* Toronto House of Anansis Press

Berns, C. (2004). Bibliotherapy: Using books to help bereaved children. *Journal of Death and Dying, 48*(4), 321–336. cognitive bibliotherapy. *Journal of Creativity in Mental Health, 5*(4), 426–439.

Chambers, A. (1990): *The Reader in the book* . In Peter Hunt (Ed) *Children's Literature*: *The Development of Criticism*. London Routledge 91-113.

Cleveland, A. (2008): *Bibliotherapy for all: Using Children's Literature about loss and grieving to increase awareness developing coping skills and build community among elementary school students*. St. Louis Missouri.

Corcoran, B., & Evans, E. (1987): *Readers. Texts, Teachers*. Milton Keyness: Open University Press.

Cuddon, J. A. (1991): *A Dictionary of Literary Terms and Literary Theory*: Cambridge Blackwell.

Gardenar, M. (1980). *Bibliotherapy: Good book or media selection plus individual guidance plus a definite goal*. (ERIC Document Reproduction Service No. ED 191 484).

Graethouse, P. A. (2017) Effects of a positive youth development approach to literacy through young adult literature in the secondary remedial reading class: an action research study. In Educational Action Research Volume 26, Issue 2

Jalongo, M. R. (1983). Bibliotherapy: Literature to promote socioeconomic growth. *The Reading Teacher, 36(8)*, 796-803.

Kamalie, L. M. (2002): *The Application of Bibliotherapy with primary school children leaving in a violent society*. University of Western Cape.

Karnowski, L. (1997): *Reconsidering teachers' roles and procedures*: *Developing dialoguing skills* in N. Karolides (Ed) Reader Response in Elementary Classrooms.

Kennedy, X. J., & Dana Giota (2010): *Literature an Introduction to Fiction, Poetry, Drama and Writing.* New York: Dell.

Maich, K.., &Kean. S. (2004) Read two Books and write me in the morning. Bibliotherapy for social emotional interaction in the inclusive classroom. Teaching exceptional Children plus 1(2




© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 26.05.2020; Accepted 28.05.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Momanyi, C., na Timammy .R. (2011) Wahariri :*Takrima Nono na Hadithi nyingine*. Longman Kenya.

Morawski, C., &Brunhuber, B. (1995). Teachers' early recollections of learning to read: Applications inreading teacher education inthe con tent areas. Reading Research and Instruction, 34, 315-331.

Namu, G.M. (1991): *Bibliotherapy for the hearing impaired in Kenya*. Unpublished Masters Thesis Kenyatta University Kenya.

Natalie, H.W. (2010): *The Effects of bibliotherapy with Zhuang Zi's fables on various aspects of stress in students-* University of Hull. New York, NY: Peter Lang Publishing, Inc.

Oluwaseye. A. J. (2017). *Bibliotherapy*: Reference and Electronic Resources librarian at Michael and Cecilia Ibru University, Agbarha-Otor,Delta State, Nigerian

Pehrsson, D. E., & McMillen, P. S. (2010). *Bibliotherapy in counseling practice*. Teaching Module for counselor education course, CED 703, at University of Nevada, Las Vegas.

Peterson,N.J.(1997) Toni Morrison : Critical and Theoretical Approaches John Hopkins University Press

Prater M.A., Johstun M.L., Pyches T.T., & Johnstun M.R. (2006) Using Childrens Books as Bibliotherapy for at risk students: A guide for teachers Preventing school failure 150(4) 5-13.

Rosenblatt L. (1995): First Published (1939): *Literature as Exploration*. New-York The Modern Language Association of American.

Rosenblatt, L. (1978) *The Reader,The text, The poem: The transaction theory of the literary work* Carbondale, Southern Illionois Press.

Sullivan A.K & Strang H.R (2002) Bibliotherapy in the Classroom: Using Literature to promote the development of emotional intelligence childhood education, 79(2) 74-80

Taft, R. J., Hotchkiss, J. L.and Lee, D. (2016) Efficacy of music therapy and bibliotherapy as interventions in the treatment of children with EBD: A literature review. *International Journal of Learning, Teaching and Educational Research,* 15, 114–129.

Todahl, J., Smith T.E., Barnes, M., & Pereira M, G, A (1998) Bibliotherapy and Perceptions of death by young children. *Journal of poetry therapy* 12(4)95-107 Duncan (2010) Goddard 2011) Cook na Wengine (2006) Thomson & Trice

Walibora K.,. na Mohammed S.A (2007): *Damu Nyeusi na Hadithi nyingine*. NRB Maximillan Publishers Ltd.

Walibora, K., na Mohammed S.A. (2007): *Kiti cha Moyoni na Hadithi nyingine*.Oxford University Press.

Wamitila, K.W. (2004): Mhariri: *Mayai Waziri wa Maradhi* Nairobi Focus Publishers.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org